ZABURI 79

Siku ya Mungu ya 27, Mwaka A

Patient Joseph Bwirhode



1. Ulingoa mzabibu toka Misri,
   ukawafukuza mataifa, ukaupanda;
   kwake ukapalia udongo, tayari,
   nao ukatoa mizizi, ukaijaza nchi.

2. Kwanini umebomoa kuta zake,
   ili wote wanaopita njiani wachume zabibu zake?
   Ili nguruwe wa mwituni auharibu,
   na wanyama wa porini wautafune?

3. Ee Mungu wa majeshi, urudi,
   uangalie toka mbinguni, uone,
   uje kuutazama mzabibu huo.
   Uulinde huo uliopanda kwa mkono wako wakuume,

4. Hatutakuacha tena hata kidogo,
   utatutunzia maisha, nasi tutaomba jina lako.
   Ee Bwana, Mungu wa majeshi, utusimike tena,
   uangazishe uso wako, nasi tutaokoka.